

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

*Simu:* +255 026 23222761-5  
*Fax No.* +255 026 2322624  
**E-mail:** [info@bunge.go.tz](mailto:info@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUANZA KWA  
VIKAO VYA KAMATI ZA BUNGE TAREHE 16 HADI 29  
JANUARI, 2017, MJINI DODOMA**

---

**1.0 UTANGULIZI**

Kamati za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana Jumatatu tarehe 16 hadi tarehe 29 Januari, 2017 Mjini Dodoma kutekeleza majukumu yake kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Sita wa Bunge uliopangwa kuanza tarehe 31 Januari 2017. Kufuatia ratiba hiyo ya shughuli za Kamati, Waheshiwa Wabunge wote wanapaswa kuwa wamewasili Mjini Dodoma ifikapo Jumapili tarehe 15 Januari, 2017 tayari kwa kuanza vikao vya Kamati. katika kipindi chote hiki cha vikao hivyo, shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Kamati ni kama ifuatavyo:

**a) ZIARA ZA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO**

Katika utekelezaji wake wa majukumu, Jumla ya Kamati 12 zitafanya ziara za kukagua miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini inayotekelezwa na Wizara/Idara zinazosimamiwa na Kamati husika. Ziara hizo zitafanyika kuanzia, Tarehe 17 hadi 21 Januari, 2017 kabla ya kuendelea na vikao tarehe 23 Januari, 2017 Mjini Dodoma.

## **b) KUPOKEA MAONI YA WADAU WA MISWADA MBALIMBALI**

Kamati mbili (2) za Kisekta zitajadili Miswada Mitatu ya Sheria ambapo **Kamati ya Katiba na Sheria** itajadili Miswada **miwili** ambayo ni:

- i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 4 wa Mwaka, 2016 [**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2016**] na Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wa Mwaka, 2016 (**The Legal Aid Bill, 2016**). Kamati hiyo itakuwa na vikao vya kupokea maoni ya wadau kuhusu Miswada hiyo siku ya **tarehe 19 na 20 Januari, 2016** Katika ukumbi wa **Serengeti** ulipo katika **Jengo la Hazina Ndogo** Mjini Dodoma kuanzia **saa tatu kamili (3:00) asubuhi hadi saa Tisa(9:00) Alasiri**
- ii) Kamati nyingine ni Kamati ya **Huduma na Maendeleo ya Jamii** ambayo itachambua Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalam wa Afya shirikishi wa Mwaka 2016 (**The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016**) na itakuwa na vikao vya kupokea maoni ya wadau kuhusu Muswada huo siku ya **tarehe 18 Januari, 2017** Katika ukumbi ulipo Jengo la Utawala Annex kwenye Viwanja vya Bunge Mjini Dodoma kuanzia **saa tatu kamili (3:00) asubuhi hadi saa Tisa (9:00) Alasiri.**

**Wadau wote katika Miswada tajwa hapo juu wanakaribishwa kufika mbele ya Kamati kutoa maoni yao katika tarehe na muda uliotajwa.**

**c) KUPOKEA TAARIFA ZA KIUTENDAJI WA WIZARA**

Aidha kuanzia tarehe 23 hadi 27 Januari, 2017, Kamati za kisekta zitaendelea kupokea Taarifa za kiutendaji wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati hizo kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) (c) na (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo Januari, 2016.

Ratiba zote za Shughuli za Kamati za Bunge ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo kamati hizo zitafanya ziara, pamoja na Miswada itakayo shughulikiwa na Kamati katika kipindi hiki vinapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz).

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano  
Ofisi ya Bunge  
**DODOMA**

13 Januari, 2017.